# Mwongozo wa kutumia chujio



## Maji safi, maisha mazuri

# Imeundwa na







A Mfuniko wa juu
B Ndoo ya juu
C Mfuniko cha chini
D Ndoo ya chini
E Chujio ya juu (kitambaa)
F Chujio gumu la ndani
G Mpira wa kuzuia maji kupenya
H Nati ya chujio
I Mrija wa kusafirisha maji
J Nati ya bomba la kumimina maji
K Mpira wa kuzuia maji
L Bomba la kumimina maji
M Padi/dodoki la kusafisha
N Kipimo cha mwisho wa chujio kufanya kazi



Huitaji kifaa chochote

# Jinsi yakufunga kifaa chako

**1**




Ondoa nati ya chujio kutoka kwenye chujio gumu.

**2**




Unganisha mrija wa kusafirisha maji kwenye chuchu/mdomo wa chujio na hakikisha inabana.

**3**




Usisukume chujio, ila zungusha ili kuepuka kuivunja na hakikisha inabana

Funga chujio ikiwa na mpira na mrija wa maji katika ndoo ya juu na mfuniko wa chini. Hakikisha mpira uko katikati ya chujio na kitako cha ndoo.




Kaza chujio kwa kutumia nati ya chujio.




Fungua nati ya bomba la maji.
Usitoe mpira kwenye bomba.




Funga bomba ikiwa na mpira kwenye tundu lililo kwenye ndoo ya chini. Kaza bomba kwa kutumia nati ya bomba.




Unganisha/weka ndoo ya juu pamoja na mfuniko wa ndoo ya chini, chujio na mrija wa maji uwe katika ndoo ya chini.

## 8




Valisha chujio la kitambaa juu ya chujio gumu na kufunika na mfuniko wa juu.

## 9




Lita 20 za maji ya kwanza yaliyochujwa yam wage.

## 10



Weka filta yako katika sehemu salama ndani ya nyumba yako. Hakikisha watoto wasichezee na itunzwe kwa uangalifu mkubwa, tofauti na hapo filta yako itaharibika.

Kifaa chako kiko tayari kwa matumizi.

# Inafanyaje kazi?



Maji machafu yana wekwa kwenye chombo cha juu ambapo kuna kifaa cha kuchuja (kandle). Filta inatumia saa 3-5 kusafisha ndoo moja nzima ya maji machafu. Maji safi yatatunzwa katika chombo cha chini. Kikihakikisha kuwa maji hayatachafuliwa, maji yanaweza kutunzwa muda mrefu unaotaka.

---

# Utunzaji wa filta

1



E

Kuzuia chujio gumu kuchafuka , chujio limefunikwa na chujio la kitambaa linalooshwa.

2



Kifaa hiki kimefunikwa na kifaa kinachoweza kutolewa kwenye filta na kuoshwa kwa maji safi na kurudishwa mahali pake.

## 3




Osha chujio gumu kila mara na kitambaa kisafi au mswaki. Usitumie sabuni.

## 4



Baada ya muda, maji yanapungua kasi ya kutiririka, chukua dodoki la kusafisha, safisha taratibu chujio gumu kuondoa ute mdogo mdogo kwenye chujio.

## 5




Kwa kutumia kipimo cha plastiki cha kuangalia mwisho wa kutumika kwa chujio, unaweza kujua wakati wa kubadilisha chujio. Kipimo kikiingia kwenye upana wa chujio basi chujio halina uwezo wa kutoa maji safi na salama na kitahitaji kubadilishwa.

# Kubadilisha chujio la maji

**1**




Fungua nati ya chujio.

**2**



Fungua kwa uangalifu chujio chafu/iliyokwisha.

**3**




Ondoa chujio iliyokwisha. Vuta mrija wa maji taratibu kutoka kwenye chujio.

**4**




Chukua chujio jipya kutoka kwenye kasha, Ondoa nati ya chujio kutoka kwenye chujio gumu.

## 5




Unganisha mrija wa kusafirisha maji kwenye chuchu/mdomo wa chujio na hakikisha inabana.

## 6




Funga chujio ikiwa na mpira na mrija wa maji katika ndoo ya juu na mfuniko wa chini. Hakikisha mpira uko katikati ya chujio na kitako cha ndoo.

## 7



Kaza chujio kwa kutumia nati ya chujio.

## 8



Unganisha/weka ndoo ya juu pamoja na mfuniko wa ndoo ya chini, chujio na mrija wa maji uwe katika ndoo ya chini.

**9**




Valisha chujio la kitambaa juu ya chujio gumu na kufunika na mfuniko wa juu.

**10**




Lita 20 za maji ya kwanza yaliyochujwa yamwage.

**11**



Kifaa chako kiko tayari kwa matumizi.

# Huondoa mchanga

# Ladha nzuri

# Ni salama

Huondoa mchanga na huleta ladha nzuri na haina gharama kubwa kulinganisha na maji ya kuchemsha. Maji salama kutoka kwenye kifaa hicho inasaidia kujikinga na magonjwa kama:

- Kuhara
- Kipindupindu
- Minyoo
- Na magonjwa mengine yatokanayo na kunywa maji machafu

Kwa maswali kuhusu kubadilisha chujio, wasiliana na muuzaji aliye karibu nawe.

www.basicwaterneeds.com

Basic Water Needs